



# COLORADO

## State Board of Education

201 East Colfax Avenue  
Denver, CO 80203-1799

Angelika Schroeder  
Chairwoman  
2<sup>nd</sup> Congressional District

Steve Durham  
Vice-Chairman  
5<sup>th</sup> Congressional District

Val Flores  
1<sup>st</sup> Congressional District

Jane Goff  
7<sup>th</sup> Congressional District

Rebecca McClellan  
6<sup>th</sup> Congressional District

Joyce Rankin  
3<sup>rd</sup> Congressional District

Debora Scheffel  
4<sup>th</sup> Congressional District

### Kumbukumbu ya Kutafsiriwa ya Shule ya Upili ya Aurora Central

#### TAARIFA YA KIPINDI CHA MAONI YA UMMA YALIYOANDIKWA KWA AJILI YA USIKILIZAJI WA UWAJIBIKAJI UNAOKUJA NOVEMBA KWENYE MIKUTANO YA BODI YA ELIMU YA JIMBO YA COLORADO

Bodi ya Elimu ya Jimbo ya Colorado inatafuta mapendekezo kutoka kwa familia, wafanyakazi wa shule na wanajamii kuhusu usikilizaji ujao wa uwajibikaji pamoja na Bodi ya Elimu ya Jimbo ya Shule ya Upili ya Aurora Central. Washiriki wa umma wanaweza:

- kutoa maoni juu ya utekelezaji wa hatua zilizoamuriwa hapo awali (jinsi shule imebadilika tangu majira ya joto ya 2017) na
- kutoa mapendekezo kuhusu hatua zaidi zilizoelekezwa na bodi (ni jambo gani linalopaswa kufanywa tunaposonga mbele).

Mnamo 2017, kama sehemu ya harakati ya mfululizo wa matukio ya uwajibikaji, Bodi ya Elimu ya Jimbo ilielekeza Shule za Umma za Aurora kutekeleza Mpango wake wa Uvumbuzi wa 2016 kwa msaada wa uongozi wa mbia wa nje (MassInsight).

Kwa habari zaidi za msingi kuhusu harakati ya mfululizo wa matukio ya uwajibikaji, tafadhali angalia: [Hati Taarifu ya CDE ya Mfululizo wa matukio ya Uwajibikaji](#) [CDE Accountability Clock Fact Sheet](#).

Kwa habari kuhusu usikilizaji wa uwajibikaji wa hapo awali wa shule hizi, ikiwemo mpango uliowasilishwa mnamo 2017, tafadhali tembelea [Tovuti ya Hatua za Uwajibikaji wa Bodi ya Jimbo](#) [State Board Accountability Actions webpage](#).

Maoni yanaweza kuwasilishwa kwa njia ZOZOTE zifuatazo:

- Kwa kukamilisha utafiti mfupi wa mtandao [short online survey](#).
- Kwa kutuma barua pepe kwa [state.board@cde.state.co.us](mailto:state.board@cde.state.co.us).
- Kwa kuwasilisha kwa maandishi kwenye Ofisi ya Bodi ya Elimu ya Jimbo: State Board Office, 201 E. Colfax, Room 500, Denver, CO 80203.

**Tarehe ya mwisho kwa ajili ya maoni yaliyoandikwa ni Jumatatu, Nov. 11, 2019 saa 6 (adhuhuri).** Maoni yatakusanywa na Ofisi ya Bodi ya Elimu ya Jimbo na kutumwa kwa wanachama wote wa Bodi ya Jimbo. Mapendekezo yote yatakuwa sehemu ya rekodi rasmi ya



usikilizaji na kuchapishwa hadharani. Maoni yanayowasilishwa kwa lugha zingine isipokuwa Kiingereza yatatafsiriwa katika Kiingereza wakati ukiruhusu. Maoni yatakayopokewa baada ya tarehe ya mwisho hayatajumuishwa katika rekodi au kupelekwa kwa Bodi ya Jimbo.

